MUHTASARI

# MIONGOZO YA HIARI KWA AJILI YA KUHAKIKISHA UVUVI MDOGOMDOGO ULIO ENDELEVU KWA MUKTADA WA USALAMA WA CHAKULA NA KUONDOA UMASKINI



Imechapishwa na
**International Collective in Support of Fishworkers (ICSF)**
27 College Road Chennai 600 006,
India

Simu: (91) 44-2827 5303
Fax: (91) 44-2825 4457
Barua pepe: icsf@icsf.net
Website: www.icsf.net

ICSF ni Asasi ya ya kimataifa inayojishughulisha na masuala yanayowahusu jamii inayofanyakazi katika sekta ya uvuvi ulimwenguni kote. Asasi hii inatambulika na Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa i na pia imo katika Orodha Maalum ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) ya mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali. Pia ina hadhi ya ushirikiano na FAO.
Kama mtandao wa kimataifa wa waraghbishi wa jamii, walimu, mafundi, watafiti na wanasayansi, shughuli za ICSF zinajumuisha ufuatiliaji na utafiti, mawasiliano na mafunzo, kampeni, harakati, pamoja na jamii husika.

**2016**

Mchoro kwa
**Frances Wild and Ella Khafaji'**

Tafsiri na
**Ali Thani, Baraka Kalangahe (Mwambao Coastal Community Network, Tanzania) and Rosemarie Mwaipopo, University of Dar es Salaam and Member, ICSF**

ISBN 978 93 80802 56 5

MUHTASARI

# MIONGOZO YA HIARI KWA AJILI YA KUHAKIKISHA UVUVI MDOGOMDOGO ULIO ENDELEVU KWA MUKTADA WA USALAMA WA CHAKULA NA KUONDOA UMASKINI

Miongozo ya hiari kwa ajili ya Kuhakikisha Uvuvi mdogomdogo ulio endelevu katika muktadha wa Usalama wa Chakula na Kuondoa Umaskini uliasisiwa na nchi wanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) na kupitishwa rasmi mwezi Juni 2014 kama chombo cha kimataifa

Umuhimu wa miongozo hii unatokana na ukweli kuwa uandaaji wake ulisukumwa na historia ya muda mrefu sana ya mapambano ya wanaojishirikisha katika sekta ya uvuvi mdogomdogo duniani kote, wakitaka hadhi na mchango wao katika sekta ya uvuvi kutambulika kama inavyostahili katika nchi zao.

Pamoja na kwamba, duniani kote, wavuvi wadogo ni uti wa mgongo wa uchumi wa sekta ya uvuvi, lakini mara nyingi wamekuwa wakipuuzwa na kubaguliwa katika mchakato wa kuifanya sekta ya uvuvi iwe ya kisasa. Licha ya hali hiyo, sekta ya uvuvi imebaki kuendelea kuimarika na yenye ustawi katika nchi nyingi.

Hata hivyo, kwa miongo kadhaa ya utelekezaji huu ikiwa ni pamoja na kwamba wavuvi wadogo wanachangia asilimia kubwa ya samaki wanaovuliwa, hata hivyo katika nchi nyingi, jamii ya za wavuvi wadogo zimebaki kuwa maskini, kuachwa nyuma, kunyimwa haki zinazowastahikia kwa ajili ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni


Hivyo, miongozo hii, inadhihirisha kutambuliwa kwa ukweli huu na nchi wanachama wa Shilika la Chakula Duniani (FAO) aidha, ni jitihada za kurudisha uvuvi mdogomdogo kwenye kitovu cha maendeleo na usimamizi wa uvuvi

Asasi ya ICSF ni miongoni mwa asasi za kiraia zilizokuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa uandaji wa Miongozo hii, unazingatia mchakato shirikishi kwa hali ya juu. Kutokana na hili, Shirika la Chakula Dunia limetambua rasmi Miongozo hii kama kumbukumbu ya Chandrika Sharma, Katibu Mtendaji wa ICSF, ambaye alikuwa bingwa wa haki za wavuvi wadogo wadogo duniani kote. Bi Sharma alipotea tangu ndege ya Shirika la ndege la Malaysia [MH 370] ilipotoweka Machi 2014; Alikuwa njiani kwenda Mongolia kwa ajili ya mkutano wa Shirika la Chakula Duniani FAO kuhamasisha uungwaji mkono kwa ajili ya kupitishwa kwa miongozo hii.

Miongozo hii ina zaidi ya vifungu 100 ambavyo vimegawanywa katika sehemu 13 na ni muhtasari wa yaliyomo katika Miongozo. Muhtasari huu umeandaliwa na ICSF na John Kurien, mwanachama mwanzilishi wa ICSF, ambaye kwa miongo minne iliyopita, amekuwa akifanya kazi na jamii za wavuvi wadogo wadogo katika maeneo mengi duniani kote, hasusani Kerala, India.

## DIBAJI

Miongozo ya Uvuvi Mdogomdogo endelevu imetengenezwa kama nyongeza ya Kanuni za Maadili ya Uvuvi unaowajibika, zilizoundwa na Shirika la Chakula Duniani mwaka 1995. Miongozo hii inaangalia uvuvi mdogomdogo na shughuli zote zilizopo katika mfumo mzima wa kuongeza thamani au tija katika sekta hiyo na jinsi unavyowahusisha wanaume na wanawake. Uvuvi mdogomdogo huchangia nusu ya samaki wanaovuliwa duniani na huajiri asilimia 90 ya wavuvi na wafanyakazi wengine katika sekta ya uvuvi duniani. Uvuvi mdogomdogo na jamii za wavuvi huwakilisha sekta yenye sifa mbalimbali na mifumo inayobadillika kwa haraka kutegemea na mahali inapoendeshwa. Kwa ujumla shughuli za uvuvi huendeshwa na kaya ambazo zimejikita katika kazi za uvuvi na jamii zake. Lakini wavuvi wadogo wameendelea kuwachwa nyuma, na umaskini katika jamii hizi umekuwa ni wa hali nyingi. Hivyo, katika kuhakikisha kuwa mchango wa uvuvi mdogomdogo katika sekta nzima ya uvuvi unakuwa mkubwa imekuwa na changamoto nyingi. Miongozo hii imeundwa a kwa mchakato shirikishi na wa mashauriano ya kipekee. Upo sambamba na unakuza viwango vya Haki za binadamu vya Kimataifa.




## 1. MALENGO

Malengo ya Miongozo hii ni kuhakikisha kuwa sekta ya uvuvi mdogomdogo itaweza kufanya yafuatayo:

- kuimarisha uhakika wa chakula duniani;
- kukuza mchango wake katika hali ya kiuchumi na kijamii ya dunia kwa baadae;
- kuchangia kuboresha hali ya kijamii na kiuchumi ya walioajiriwa/kujiajiri katia sekta ya uvuvi; na,
- kufanikisha matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

Miongozo hii inatakiwa kuongeza uelewa wa umma juu ya jukumu, mchango na uwezo wa wavuvi wadogo wadogo.

Malengo hayo hayana budi kutimizwa kwa mtazamo unaoendeleza haki za binadamu. Hivyo jamii za wavuvi wadogo wadogo zinapaswa kupewa uwezo wa kushiriki katika mchakato wa kutoa maamuzi, na kubeba wajibu wa kusimamia uvuvi endelevu.



## 2. ASILI NA UPEO

Miongozo hii ni ya hiari na ni ya wigo wa kimataifa, na inazilenga nchi zinazoendelea. Inatakiwa kutambulika na wadau katika maeneo yote ya uvuvi – ikiwemo uvuvi wa bahari, maziwa na mito, na inalenga wadau wote wanaohusika na uvuvi – yaani:- mataifa; asasi zisizo za kiserikali za kimataifa, asasi zisizo za kiserikali za kitaifa, vyama vya kiraia, taasisi za elimu na sekta binafsi

Miongozo hii inatambua kuwa sekta ya uvuvi mdogomdogo ina mchanganyiko mkubwa - wa mbinu na washiriki - na ni vigumu kuwa na tafsiri inayofanana kwa mataifa yote. Kwa hiyo, kwa kutumia viwango vinavyowekwa na miongozo hii, mataifa yanashauriwa kutumia njia shirikishi ili kupata tafsiri inayokubalika ya uvuvi mdogomdogo na kuwatambua wale waliosahaulika na waliochwa nyuma zaidi kushirikishwa katika sekta hii. Miongozo hii inapaswa kutafsiriwa na kutumika kwa mujibu wa mifumo ya kisheria ya kitaifa na taasisi.



## 3. MIONGOZO YA MSINGI

Mwongozo huu una msingi mikuu 13. Ambayo inaendana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, vinavyojali majukumu ya uvuvi na shughuli za maendeleo endeleevu kwa kuyazingatia makundi yaliyosahaulika na kuachwa nyuma kimaendeleo pamoja na haja ya kusaidia kuendelea kutambua haki ya kupata chakula cha kutosha

Misingi hiyo inajumuisha:

01. haki za binadamu na utu;
02. heshima ya mila na tamaduni;
03. kutobaguliwa;
04. nafasi ya mwanamke katika usawa na haki za kijinsia;
05. haki usawa kwa wote;
06. mashauriano shirikishi;
07. utawala wa sheria;
08. uwazi;
09. uwajibikaji;
10. uendelevu wa kiuchumi, kijamii na kimazingira;
11. mbinu za kiujumla na jumuishi;
12. wajibu wa kijamii; na
13. uwezekano wa uwepo uchumi mzuri wa kijamii.

# 4. UHUSIANO NA VYOMBO VINGINE VYA KIMATAIFA

Miongozo ya Uvuvi Mdogomdogo ulio Endelevu inapaswa kutafsiriwa na kutumiwa kulingana na haki na wajibu wa sheria za kitaifa na kimataifa na kwa kuzingatia ahadi za hiari chini ya vyombo husika vya kikanda na kimataifa.

Miongozo hii inaweza kutumika kuongoza marekebisho na kuchochea uundaji wa sheria na kanuni mapya au za nyongeza. Hata hivyo, vipengele katika miongozo visisomeke kama vikwazo au kudhoofisha haki au majukumu yoyote ambayo serikali inaweza kuwa nayo chini ya sheria za kimataifa.



# 5. USIMAMIZI WA MAENEO KATIKA UVUVI MDOGOMDOGO NA USIMAMIZI WA RASILIMALI

## A. KUWAJIBIKA KATIKA USIMAMIZI WA UMILIKI WA RASILIMALI

Kuwajibika katika usimamizi wa umiliki wa rasilimali i ni muhimili kwa mafanikio ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni na kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinatimizwa kwa jamii za wavuvi wadogo.

Jamii ya wavuvi wadogo inapaswa kuwa na haki kamili za kumiliki rasilmali za uvuvi kwa kuzingatia usawa na utambuzi wa tamaduni zao. Hii ni pamoja na haki ya kumiliki maeneo ya uvuvi, ardhi na misitu iliyokaribu. Ni muhimu kwa haki hii kuzingatia haki ya wanawake. Mifumo yote ya haki itambuliwe kihalali, iwekwe kwenye kumbukumbu na kuzingatiwa.

Ufuatiliaji wa haki hizi ni muhimu upewe utambuzi wa kisharia, hususan kwa kuzingatia haki za kimila na kutoa kipaumbele kwa malihai za bahari na mito na ardhi za wenyeji/wazawa na jamii ndogo. Pale ambapo sheria itaainisha haki za wanawake, ni muhimu kuwa zianishwe kwenye mfumo mzima wa miliki.

Ni muhimu kutambua wajibu wa jamii za wavuvi wadogo wadogo na wenyeji/wazawa kurejesha, kuhifadhi, kulinda na kusimamia kwa pamoja ikolojia ya mito na pwani.

Katika maeneo ambayo taifa linamiliki au kudhibiti ardhi na rasilimali za bahari na mito, haki zao za umiliki zinapaswa kuanzishwa kwa kutilia maanani malengo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira, hususani, kuzingatia matumizi na usimamizi wa pamoja jamii za wavuvi wadogo.

Haki maalum kwa wavuvi wadogo kuvua katika bahari na mito ya nchi imeingizwa katika Kanuni za Maadili ya Uvuvi Uliowajibika (Ibara 6.18) za Shirika la Chakula Duniani (FAO). Kwa kuzingatia hili, ni muhimu kwa nchi kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wavuvi wadogo. Hii iwe ni kabla ya kuwekeana mikataba na makundi mengine (km wavunaji wakubwa) ili haki ta matumizi ya rasilmali hizi za wavuvi wadogo ziheshimiwe.

Watumiaji wengine wanaongeza ushindani katika maeneo ya wavuvi wadogo, na kusababisha migogoro. Nchi zinapaswa kuhakikisha kwamba jamii za wavuvi wadogo wanapewa kinga maalum na hawahamishwi kiholela au kwamba haki zao

halali za umiliki haziingiliwi kuondolewa. Katika suala la miradi ya maendeleo mikubwa, nchi pamoja wa wahusika wengine wanapaswa kufanya mashauriano pamoja na tathimini ya madhara yatokanayo na athari hizi kwa jamii za wavuvi wadogo.

Migogoro ya haki ya umiliki inayohusisha jamii ya wavuvi wadogo ni muhimu kutatuliwa na serikali kwa wakati, gharama nafuu na ufanisi na pia iruhusu suluhisho ikiwa pamoja na kurejeshewa, kinga, fidia kila inapobidi kutekelezwa mara moja.

Majanga ya asili na/au migogoro ya kivita ambayo husababisha uhamisho wa lazima kwa jamii za wavuvi wadogo inaendelea kauthiri maisha yao sehemu nyingi. Ili kupunguza athari hizi, ni muhimu kwa nchi kucuhukua kila hatua kwarejeshea jamii hizi maeneo yao ya mavuvi na maeneo ya pwani ili kuwezesha uendelevu wa uvuvi huu. Katika mazingira haya, mbinu za kuwahimili jamii ambazo zimeathirika vibaya na ukiukwaji wa haki za binadamu zichukuliwe pamoja na kukabiliana na ubaguzi wowote dhidi ya wanawake katika umiliki wa maeneo haya.

## B. USIMAMIZI ENDELEVU WA RASILIMALI

Ni muhimu kwa hatua kuchukuliwa kwa ajili ya hifadhi ya muda mrefu na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, aidha mahitaji na fursa ya wavuvi wadogo zinabidi kutambuliwa. Haki ni budi kuendeana na wajibu. Haki ya kumiliki zipewe uwiano na uhifadhi na matumizi endelevu ya mavuvi.

Wavuvi wadogo wanapaswa kutumia mbinu endelevu za uvuvi ambazo hazina madhara kwenywe mazingira na viumbe hai vya majini. Nchi zinapaswa kusaidia uvuvi mdogomdogo kuchukua jukumu la usimamizi wa rasilimali. Nchi zinapaswa kuhusisha jamii katika kubuni, kupanga na kutekeleza mikakati ya usimamizi, kuhakikisha ushiriki sawa wa wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Nchi zinapaswa kuendeleza mifumo shirikishi ya usimamizi kulingana na sheria za kitaifa.

Nchi zinapaswa kubuni mifumo ya ufuatiliaji, udhibiti na uangaliazi iliyo bora na inayoendeana na uvuvi mdogomdogo. Nchi zinapaswa kujitahidi kuepusha, kuzuia na kutokomeza mbinu zote za uvuvi zilizo haramu na haribifu; na wavuvi wadogo wadogo wanapaswa kuwezesha mifumo ya ufuatiliaji kutumika ikiwa ni pamoja na kushirikiana na ngazi za usimamizi za katika sekta ya uvuvi.

Nchi zinapaswa kufafanua wajibu na majukumu ya pande zote zinazounda mfumo wa usimamizi shirikishi, kwa kufuata michakato inayokubalika kisheria. Wavuvi wadogo wawakilishwe katika vyama na vyombo husika vya kitaalamu katika ngazi zote ili waweze kushiriki katika kufanya maamuzi na kuundaji wa sera.

Katika kukuza usimamizi shirikishi, nchi pamoja na wavuvi wadogo wanapaswa kuwawezesha wanawake na wanaume wanaoshiriki katika uvunaji na hatu zingine katika mfumo wote wa thamani wa uvuvi mdogomdogo ili waweze kuchangia maarifa, maoni na mahitaji yao katika sekta hii.

Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa haki ya umiliki wa mavuvi za jamii za wavuvi wadogo watumiao maeneo yaliyo kwa mipaka y amaeneo ya majini yanayoingiliana na nchi mbalimbali zinalindwa.

Nchi zinapaswa kuepuka hatua za kisera na kifedha zinazochangia kuzidisha viwango vya uvuvi ambavyo vitaathiri ustawi wa wavuvi wadogo.



## 6. MAENDELEO YA JAMII, AJIRA NA USALAMA KAZINI

Wahusika wote wanapaswa kuchukua mtazamo wa kiujumla juu ya maendeleo na usimamizi wa uvuvi mdogomdogo. Nchi zinapaswa kukuza uwekezaji katika sekta za afya, elimu, kusoma na kuandika, ikiwemo digitali na ujuzi mwengine wa kiufundi.

Nchi zinapaswa kukuza mipango ya hifadhi za jamii kwa ajili ya sekta ya uvuvi mdogomdogo, na washirika wake wotte katika mfumo mzima mzima wa thamani. Nchi zinapaswa kuendeleza miradi kwa ajili ya kuweka akiba, mikopo na bima, pamoja na msisitizo juu ushirikishwaji na upatikanaji wa huduma hizi kwa wanawake.

Wahusika wote wanapaswa kutambua kuwa shughuli mbalimbali katika mnyororo wa thamani ya uvuvi mdogomdogo kuwa ni shughuli za kiuchumi na kitaaluma.

Nchi zinapaswa kuzingatia ajira zenye utu.

Nchi zinapawsa kuhakikisha kuwa haki za wavuvi na wafanyao kazi za uvuvi zinatambuliwa hadi wanapofikia kiwango kizuri cha ubora wa maisha. Nchi zinapaswa kufuata njia zisizo za ubaguzi na sera bora za kiuchumi ili wafanyakazi hawa wapate mapato yanyowiana na kazi zao, mitaji na usimamizi wao. Nchi na wahusika wengine wanapaswa kusaidia fursa mbadala za kukuza mapato. Mazingira sahihi yanapaswa kuandaliwa kwa ajili ya jamii za wavuvi wadogo kufanya shughuli zinazohusiana na uvuvi.

Uhamaji ni mkakati wa kawaida wa kujikimu kimaisha. Nchi zinapaswa kutambua na kushughulikia visababishi na madhara ya nyenendo za wavuvi wanaohamahama kati ya mipaka ya nchi kadhaa.

Nchi zinapasa kushughulikia afya, usalama na mazingira ya kazi yasiyoridhisha. Nchi pia zinapaswa kuzuia ajira za kulazimishwa na utumwa unaotakana na madeni.

Nchi zinapaswa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za shule na vifaa vya elimu, kutambua umuhimu wa ustawi na elimu ya watoto kwa maisha yao ya baadaye.

Uzito wa hali ya usalama katika bahari, maziwa na mito na sababu mbalimbali zinazoletetleza hali hii zinapaswa kutambuliwa na wahusika wote.

Ni muhimu kujua, usalama na uhakika wa afya kazini wa wavuvi wadogo vinajumlishwa katika utaratibu mzima wa usimamizi wa uvuvi.

Nchi zinapaswa kulinda haki za binadamu na utu wa wadau wa uvuvi mdogomdogo katika nyakati za migogoro ya vita.

# 7. MNYORORO WA THAMANI BAADA YA MAVUNO (KUVUA) NA BIASHARA

Jukumu kuu la sekta ndogo baada ya mavuno au uvuvi katika sekta nzima ya uvuvi mdogo mdogo linapaswa litambulike na wadau wote. Aidha wannawake wanatika kushiriki na kupewa nafasi kubwa katika sekta ndogo baada ya samaki kuvuliwa ambapo hili vile vile linapaswa kutambulika na wadau wote.

Ni muhimu kwa serikali kuwekeza katika miundombinu sahihi, miundo ya kitaasisi na kujenga uwezo wa wavuvi katika hatua zote zihusuzo uvuvi mdogomdogo. Mifumo ya asili ya ushirikiano kati ya wavuvi na wafanyao shughuli za uvuvi itambuliwe kihalali.

Ni muhimu kama mbinu zitabuniwa za kuepusha hasara kwenye uzalishaji katika mfumo mzima wa thamani katika uvuvi mdogomdogo. Nchi zinapaswa kukuza biashara yenye usawa na isiyo ya kibaguzi ya bidhaa za wavuvi wadogo katika masoko ya ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa. Lakini, ni muhimu kuwa makini katika uendelezaji wa biashara ya kimataifa ya mazao ya uvuvi ili isiathiri mahitaji ya lishe ya jamii zinazotegemea samaki kwa ustawi wake kiujumla.

Faida kutokana na biashara ya kimataifa inapaswa kusambazwa kwa usawa na mifumo ya usimamizi wa uvuvi inapaswa kuwekwa ili kuzuia uvunaji wa rasilmali za uvuvi usio na viwango na unaosukumwa na mahitaji ya soko.

Ni muhimu kwa tathmini za kimazingira, kijamii na zinginezo zinazohusika (miongoni mwa nyingine ) ziwe ni sehemu ya sera na taratibu zinazochukuliwa ili kuhakikisha kwamba athari zitokanazo na biashara ya kimataifa juu ya mazingira na utamaduni, uhakika wa chakula na maisha ya wavuvi wadogo yanaweza kupimwa na kushughulikiwa kwa usawa.

Serkali iwezeshe upatikanaji wa taarifa za masoko na biashara kwa wakati na zilizosahihi kwa wadau katika mfumo wa thamani wa wavuvi wadogo.

## 8. USAWA WA JINSIA

Mikakati ya uendelezaji uvuvi mdogomdogo inapaswa ianishe masuala ya haki za kijinsia. Nchi zinapaswa kuzingatia wajibu wao chini ya sheria za kimataifa za haki za binadamu na kutekeleza makubaliano ambayo wao ni wanachama yanayohusiana na masuala ya wanawake.

Hatua maalum za kushughulikia ubaguzi wa wanawake zichukuliwe. Usawa wa kijinsia ni muhimu ufikiwe kwa kuunda sera na sheria na kubadilisha zile ambazo hazilingani na lengo hili.

Mifumo ya tathmini iendelezwe ili kuangalia matokeo ya sheria, sera na mikakati inayochukuliwa koboresha hadhi ya wanawake na kupata usawa wa kijinsia.

Teknolojia bora na zilizosahihi kwa shughuli za wanawake zinapaswa ziendelezwe.



## 9. HATARI ZA MAAFA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI

Kupambana na mabadiliko ya tabia nchi kunahitaji hatua za haraka na zenye ubunifu, na tahadhari maalumu inapaswa kuzingatiwa kwa ajili ya jamii ya wavuvi wadogo wanaoishi katika visiwa vidogo. Mbinu jumuishi na ya kijumla kwa kushirikiana na sekta mtambuka inahitajika. Ni muhimu kwa mbinu za kukabilian ana majanga pamoja na misaada iwe inatolewa inavyobidi.

Wahusika wote wa majanga yanayosababishwa na binadamu na ambayo yanaathiri shughuli za uvuvi mdogomdogo wanapswa wawajibishwe. Athari za mabadiliko ya tabia nchi na majanga katika hatua baada ya uvuvi na masoko yanapaswa yazingatiwe. Dhana ya “kurekebisha kwa ubora zaidi’ inapaswa kutumika katika kukabiliana na maafa. Aidha, ni muhumu kuhimiza na kukiuza matumizi ya nishati endelevu katika mfumo zima wa uongezaji thamani.



## 10. UWIANO WA SERA, URATIBU WA TAASISI NA USHIRIKIANO

Ili kukuza maendeleo ya kiujumla katika jamii za wavuvi wadogo, nchi zinapaswa kutambua haja ya kuwa na sera zinazowiana na kujitahidi kuimarisha uwiano huo.

Nchi zinapaswa kutengeneza na kutumia mbinu za upangaji wa maeneo kwa kuzingatia maslahi ya uvuvi mdogomdogo na jukumu lake katika usimamizi wenye uwiano wa ukanda wa pwani.

Nchi zinapaswa kuchukua hatua za kisera ili kuanisha na kuoanisha mifumo na sera zinazoathiri uhai wa ikolojia ya bahari, mito na maziwa.

Sera ya uvuvi inapaswa kutoa dira ya muda mrefu kwa ajili ya uvuvi mdogomdogo ulio endelevu.
Ni muhumu kuainisha maeneo maalumu ya mawasiliano katika mamlaka za serikali na mashirika kwa ajili ya jamii za wavuvi wadogo.

Wadau wa uvuvi mdogomdogo wanapaswa kukuza ushirikiano miongoni mwa vikundi/mashirika yao.

Nchi zinapaswa kukuza mifumo ya utawala inayochangia usimamizi bora wa uvuvi mdogomdogo. Ushirikiano wa kimataifa na kikanda unahitajika ili kupata uvuvi mdogomdogo endelevu.

## 11. MAELEZO, UTAFITI NA MAWASILIANO

Nchi zinapaswa kuanzisha, katika hali ya uwazi, mifumo ya ukusanyaji wa takwimu husika kwa ajili ya kufanya maamuzi juu ya usimamizi endelevu wa uvuvi mdogomdogo. Ufanisi wa maamuzi unahitaji mawasiliano na taarifa. Nchi zinapaswa kujitahidi kuzuia rushwa, kuongeza uwazi na kuhakikisha watoa maamuzi wanawajibika.

Jamii ya wavuvi wadogo wadogo ni wamiliki, watoaji na wapokezi wa elimu. Taarifa ambazo ni za muhimu kwa ajili ya uvuvi mdogomdogo unaowajibika, pamoja na maendeleo endelevu, zinapaswa kutolewa. Maarifa, utamaduni, desturi na teknolojia za jamii za wavuvi wadogo zinapaswa kutambuliwa na kuwekwa kwenye kumbukumbu.

Nchi zinapaswa kuunga mkono jamii za wavuvi wadogo - hasa wazawa na wanawake - wanaotegemea uvuvi kwa ajili ya kujikimu. Ni muhimu vilevile kwa mifumo sahihi na mitandao iliyopo katika ngazi ya jamii, ngazi ya kitaifa na ngazi za juu itumike kukuza ubadilishanaji na upashanaji wa taarifa katika sekta hii.

Nchi zinapaswa kutenga fedha kwa ajili ya utafiti wa uvuvi mdogomdogo na kuhimiza ukusanyaji shirikishi wa takwimu na tathmini ya sekta hii.

Nchi zinapaswa kuendeleza utafiti katika maeneo mbali mbali hasa katika muktadha wa mahusiano ya kijinsia ili kuelekeza mikakati ambayo itahakikisha usawa wa manufaa yatokanayo na mikakakti hii kwa wanaume na wanawake katika uvuvi. Nchi zinapaswa kuendeleza matumizi ya samaki katika programe za elimu kwa walaji ili kupanua utambuzi wa jukumu la uvuvi mdogomdogo, na ili kuongeza ufahamu wa faida za kiafya za kula samaki.

## 12. KUJENGA UWEZO

Uwezo wa kushiriki katika mchakato wa kutoa maamuzi uimarishwe.

Nchi zinapaswa kujenga uwezo kwa wavuvi wadogo kunufaika na fursa za masoko.

Mifumo ya kujenga uwezo inweza kuwa ni ya aina mbili, Kwanza, ni muhimu kuwa maarifa na ujuzi yaendelezwe ili kuwezesha maendeleo endelevu, na pili, ni muhimu kuwe na mipango ya usimamizi shirikishi inayofanikiwa.



## 13. KUSAIDIA UTEKELEZAJI NA UFUATILIAJI

Washirika wote wanahimizwa kutekeleza Miongozo hii ya uvuvi mdogomdogo endelevu.

Umoja wa Mataifa na Mashirika yake mahsusi yanapaswa kuunga mkono juhudi za hiari za Nchi kutekeleza Miongozo hii.

Nchi na washirika wengine washirikiane kujenga uelewa wa Miongozo hii, na kuisambaza ka matoleao rafiki.

Umuhimu wa mifumo ya ufuatiliaji inapaswa kutambuliwa. Wawakilishi halali wa jamii zaa wavuvi wadogo wanapaswa kushirikishwa katika uendelezaji na matumizi ya mikakati ya utekelezaji ya Miongozo hii na katika ufuatiliaji wake.

Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa linapasa kukuza na kusaidia maendeleo ya program ya usaidizi ya kidunia.





Nakala nzima ya Miongozo hii ya hiari kwa ajili ya kuhakikisha uvuvi mdogomdogo ulio endelevu katika muktadha wa usalama wa chakula na kuondoa umaskini inapatikana katika tovuti: http://www.fao.org/fishery/topic/18240/en



**International Collective in Support of Fishworkers (ICSF)**
27 College Road, Chennai 600 006, India

ISBN 978 93 80802 56 5